**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/2024

**ILIYOWASILISHWA NA**
**MHE. SHAMATA SHAAME KHAMIS (MBM)**
**WAZIRI WA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO**
**ZANZIBAR**

**MEI, 2023**

## YALIYOMO

UTANGULIZI ........................................................ 1

MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO... 5
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023 ........................................................ 5
Mapato Yaliyokusanywa Kulingana na Malengo Yaliyowekwa ........................ 5
Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji ........................ 6
Fedha Iliyopatikana kwa Kipindi cha Utekelezaji ........................ 8

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023. ........................ 9
PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO ........................ 10
Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji ........................ 11
Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula. ........................ 11
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ........................ 12
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI ........................ 13

PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU ........................ 14
PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO ........................ 15
Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo ........................ 15
Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI ........................ 16
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO ........................ 17
Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ........................ 17
Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ........................ 18
Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba ..... 19

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ........................ 19
Makadirio ya Mapato ........................ 19
Makadirio ya Matumizi 2023/2024 ........................ 19

PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO ........................ 20
MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024. ........................ 20
Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji ........................ 21
Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika Chakula ........................ 21
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar ........................ 22
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ........................ 23

PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU ..... 23
Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo ..... 24
Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar ..... 25
Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ..... 25
Mipango, Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ..... 26
Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba ..... 26

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ..... 27
SHUKURANI ..... 27

VIAMBATANISHO ..... 30
Kiambatanisho Nam. 1A: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2021 -2022, Zanzibar ..... 30
Kiambatanisho Nam. 1B: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2021 – 2022 ..... 30
Kiambatanisho Nam. 2A: Idadi ya Mifugo iliyokaguliwa na Kuchimjwa, 2022 ..... 31
Kiambatanisho Nam. 2B: Idadi ya Kuku waliokaguliwa na Kuchimjwa, 2022 ..... 31
Kiambatanisho Nam. 3: Uzalishaji wa Mayai na Maziwa 2022 ..... 32
Kiambatanisho Nam. 4: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu kwa Mwaka 2021 na 2022 32
Kiambatanisho Nam. 5: Upatikanaji wa Mapato Julai 2022 hadi Machi, 2023 ..... 33
Kiambatanisho Nam. 6: Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2022 Hadi Machi, 2023 ..... 34
Kiambatanisho Nam. 7A: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 ..... 35
Kiambatanisho Nam. 7B: Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 ..... 36
Kiambatanisho Nam. 8A: Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliajimaji ... 38
Kiambatanisho Nam 8B: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula39
Kiambatanisho Nam. 8C: Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC) ..... 40
Kiambatanisho Nam. 8D: Mradi wa Kudhibiti Nzi Waharibifu wa Matunda ..... 41
Kiambatanisho Nam. 8E: Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (AGRI-CONNECT) ..... 42
Kiambatanisho Nam. 8F: Mradi wa Kilimo Tija ..... 43
Kiambatanisho Nam. 8G: Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC) ..... 44
Kiambatanisho Nam. 8H: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo ..... 45
Kiambatanisho Nam. 9: Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Programu kwa Mwaka 2023/2024 ..... 46

## HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/2024

### UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, ambayo yanawasilishwa katika mfumo wa Programu (PBB).

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufikia leo tukiwa wazima na wenye afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ambapo asilimia kubwa wanajihusisha na kazi za Kilimo, Ufugaji na Uhifadhi wa Maliasili.

3. **Mheshimiwa Spika,** pili nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025. Aidha, tunazipongeza pia juhudi za Mheshimiwa Rais za kufuatilia kwa karibu utendaji wa taasisi za Serikali; kushajiisha na kuhamasisha uwekezaji katika nchi yetu kwa maslahi mapana ya Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** tatu napenda nitumie fursa hii tena kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini kwa kunipa dhamana ya kuisimamia Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo. Aidha, napenda nichukue fursa hii kumuhakikishia kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu na naahidi kwamba nitaitumikia Serikali hii kwa uwezo wangu wote kwa kusimamia vyema utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 kwa kuleta maendeleo katika sekta ya Kilimo nchini.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kumshauri vyema Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuendeleza sekta ya kilimo. Aidha, ninawashukuru kwa maelekezo na miongozo yao wanayoitoa kwa Wizara yangu siku hadi siku.

6. **Mheshimiwa Spika,** nakupongeza wewe binafsi kwa umakini na umahiri wako wa kuliendesha Baraza la Wawakilishi, pia nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaokusaidia kuliongoza Baraza hili na tunawaombea dua Mwenyezi Mungu awazidishieni uwezo, hekima na busara ili mpate wepesi wa kuliendesha Baraza kwa ufanisi na mafanikio zaidi.

7. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii adhimu kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kilimo, Biashara na Utalii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Fuoni pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushauri na miongozo wanayoitoa kwa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo katika kufanikisha utekelezaji wa malengo kwenye bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023. Aidha, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo Mwakilishi wa Wananchi wa jimbo la Mkoani, pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2023/2024. Napenda kukuhakikishia kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo waliyotupatia tumeyazingatia na kuyaweka katika bajeti hii ninayoiwasilisha.

8. **Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kuitumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Micheweni kwa kunipa mashirikiano na kuwa pamoja nami katika suala zima la kufanikisha maendeleo ya jimbo letu na ya nchi kwa ujumla. Naahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha katika maamuzi yatakayoleta maendeleo jimboni mwetu.

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo inaendeleza Mipango na Mikakati iliyoanzishwa na Serikali katika kuendeleza Sekta ya Kilimo ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapunguza utegemezi wa mahitaji ya chakula; kwa kuendeleza kilimo biashara katika uzalishaji wa mazao ya chakula na kuwawezesha vijana kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Juhudi nyengine ni kuimarisha uzalishaji wa mazao ya viungo, mboga na matunda pamoja na mazao ya mizizi ambayo ndio chachu ya maendeleo katika sekta ya viwanda na kuendeleza uzalishaji wa zao la nazi na karafuu nchini. Vilevile, upatikanaji mzuri wa huduma za mifugo ikiwemo dawa, chanjo na utoaji wa elimu juu ya ufugaji, uzalishaji wenye tija na matumizi ya mbegu bora za mifugo utaendelezwa. Wizara yangu pia itaendelea na usimamizi wa misitu ya hifadhi na ya jamii kwa lengo la kuhifadhi bioanuai, mazingira pamoja na kuimarisha huduma za utalii wa kimaumbile.

10. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo inayojumuisha mazao, mifugo na maliasili za misitu bado ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa Zanzibar na inachangia moja kwa moja kwa wananchi katika kujikimu kimaisha. Sekta ya Kilimo imeajiri takriban asilimia 40 ya wananchi wa Zanzibar na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hii katika kujikimu kimaisha. Lengo kuu la Wizara ni kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji kwa kutumia mbinu bora na teknolojia za kisasa, upatikanaji wa masoko na hatimae kukuza pato la Taifa sambamba na uhifadhi wa maliasili zetu. Kwa mwaka 2022 Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 22.9 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 24.6 iliyoripotiwa mwaka 2021.

11. **Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kwamba jumla ya eneo lililopandwa mazao mwaka 2022 limeongezeka hadi kufikia ekari 104,316 ikilinganishwa na ekari 98,591 za mwaka 2021, sawa na ongezeko la ekari 5,725. Kati ya eneo hilo, ekari 86,625 ambazo ni sawa na asilimia 83.0 zilipandwa mazao ya chakula. Zao la muhogo lilichukua eneo kubwa la ekari 34,501 ambazo ni sawa na asilimia 33.1 ya eneo lote lilopandwa mazao ya chakula kwa mwaka 2022, zao la mpunga lilipandwa katika eneo la ekari 29,086 ambazo ni sawa na asilimia 27.9, na mazao ya mboga na matunda yalipandwa katika eneo la ekari 17,691 ambazo ni sawa na asilimia 17.0 (Kiambatanisho Nam. 1A na 1B). Hivyo, Wizara inaendelea na juhudi za kuhamasisha wakulima kulima mazao ya chakula, mboga, matunda na viungo ili kutosheleza soko la ndani likiwemo la utalii sambamba na kuongeza pato la Taifa.

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kwa tofauti ya tani 13,686 kutoka tani 328,495 mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 342,181 mwaka 2022. Ongezeko hili la uzalishaji limetokana na kushajihika kwa wakulima kuongeza juhudi katika kilimo ikiwa ni pamoja na kupanda mazao yanayohimili ukame ikiwemo muhogo na maboga. Uzalishaji wa zao la muhogo umeongezeka kutoka tani 181,668 za mwaka 2021 hadi kufikia tani 202,519 mwaka 2022 na viazi vitamu vimeongezeka kutoka tani 36,812 za mwaka 2021 hadi kufikia tani 40,286 mwaka 2022. Kwa upande wa zao la mpunga, uzalishaji umepungua kidogo kutoka tani 30,353 mwaka 2021 hadi tani 27,947 mwaka 2022 kutokana na maeneo mengi kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji pamoja na kipindi kirefu cha ukavu. Aidha, uzalishaji wa mboga na matunda umeongezeka kwa tofauti ya tani 1,484 kutoka tani 64,820 mwaka 2021 hadi kufikia tani 66,304 mwaka 2022, kutokana na wananchi wengi kuhamasika na kilimo cha umwagiliaji kwenye matunda na mboga.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa zao la biashara la karafuu, uzalishaji umepungua kutoka tani 7,840.8 mwaka 2021 hadi kufikia tani 4,734.1 za mwaka 2022 ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 40. Hali hii imetokana na kuwa na msimu mdogo wa uzalishaji. Wizara inaendelea kuhamasisha wakulima wa zao hili kwa kuwataka kuongeza juhudi katika uzalishaji wenye tija kwa kuwapatia miche bora, elimu ya uoteshaji na uhuishaji.

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mazao ya mifugo, takwimu zinaonesha kuongezeka kwa uchinjaji wa ng'ombe kutoka 25,916 mwaka 2021 hadi 27,326 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 5.4 (Kiambatanisho Nam. 2A). Idadi ya kuku waliochinjwa wameongezeka maradufu hadi kufikia kuku 1,130,891 mwaka 2022 ukilinganishwa na kuku 751,073 tu mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 50 (Kiambatanisho Nam. 2B). Vilevile, uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai 15,723,843 mwaka 2021 hadi kufikia mayai 21,659,078 mwaka 2022 (Kiambatanisho Nam. 3). Idadi ya mbuzi na kondoo waliochinjwa imepungua kutoka 7,447 mwaka 2021 hadi mbuzi na kondoo 4,465 mwaka 2022. Aidha, uchinjaji wa bata umepungua kutoka bata 3,193 mwaka 2021 hadi kufikia bata 2,150 mwaka 2022 na uzalishaji wa maziwa nao umepungua kutoka lita 6,602,332 za mwaka 2021 hadi lita 5,266,987.

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mazao ya misitu, takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2022 matumizi ya kuni yameongezeka kutoka mita za ujazo 25,813 mwaka 2021 hadi kufikia mita za ujazo 26,236, sawa na ongezeko la asilimia 1.6. Matumizi ya boriti (majengo) pia yameongezeka kutoka mita za ujazo 1,422 mwaka 2021 hadi 1,741 mwaka 2022 sawa na asilimia 22.4. Aidha, uzalishaji wa mapau ya kuezekea umeongezeka kutoka mita za ujazo 2,956 mwaka 2021 hadi kufikia mita 2,970 mwaka 2022 sawa na asilimia 2.7. Uzalishaji wa nguzo kubwa umepungua kutoka mita za ujazo 3,098 mwaka 2021 hadi kufikia 2,948 mwaka 2022 (Kiambatanisho Nam. 4). Ongezeko la matumizi ya mazao ya misitu limetokana na matumizi makubwa ya shughuli za kimaendeleo ikiwemo ujenzi na upishi wa dagaa, bekari za mikate na kambi za vikosi vya Ulinzi, ambao bado unaendelea kutumia kuni kwa kiwango kikubwa. Pamoja na matumizi hayo makubwa ya kuni kiujumla, kwa upande wa wananchi hasa wa mijini matumizi ya kuni yamepungua kwa vile wamejielekeza kutumia nishati mbadala ya kupikia ikiwemo gesi na umeme. Wizara inaendelea kuhamasisha jamii kutumia mbinu mbadala kwa nishati (Gesi na Umeme) na ujenzi (Aluminium, vioo na chuma) ili kunusuru misitu na bioanuai zilizomo.

## MUUNDO NA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO

16. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo imeundwa na Idara sita (6) ambazo ni Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula, Idara ya Umwagiliaji Maji, Idara ya Misitu, Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Aidha, zipo Taasisi tatu (3) ambazo ni Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo; pamoja na Ofisi Kuu Pemba. Wizara ina jumla ya wafanyakazi wa kudumu 2,486 ambapo miongoni mwao wafanyakazi 1,900 wapo Unguja na wafanyakazi 586 wapo Pemba.

17. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina majukumu makuu yafuatayo:

    1) Kusimamia maendeleo ya uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula na biashara, huduma za pembejeo na zana za kilimo, huduma za ugani (elimu kwa wakulima) pamoja na uhifadhi na ukaguzi wa mazao;

    2) Kulinda, kuhifadhi na kusimamia rasilimali za misitu na wanyamapori;

    3) Kubuni, kupanga na kutekeleza kazi za utafiti wa sekta za kilimo (mazao, mifugo na misitu) na kutoa matokeo yake kwa wadau;

    4) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti pamoja na kuratibu mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi wakiwemo washirika wa maendeleo na sekta binafsi; na

    5) Kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala ikiwa ni pamoja na masuala ya mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu pamoja na uratibu wa masuala mtambuka ikiwemo ukimwi na jinsia.

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023

### Mapato Yaliyokusanywa Kulingana na Malengo Yaliyowekwa

18. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/23, ilikadiriwa kukusanya mapato ya TZS bilioni 4.70 kupitia vianzio vyake tisa (9) vilivyopo Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai,

2022 hadi Machi, 2023 Wizara imeweza kukusanya TZS bilioni 3.849 sawa na asilimia 82 ya makisio (Kiambatanisho Nam. 5).

**Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji**

**19. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 Wizara imepata mafanikio yafuatayo:

a. Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Cheju, Kibokwa, Kinyasini na Mlemele kwa asilimia 100 ambapo jumla ya wakulima 5,710 [Cheju 2,500; Kibokwa 1,235; Kinyasini 1,600 na Mlemele 375] wamepatiwa konde kwa kuendeleza kilimo cha mpunga;

b. Jumla ya tani 88 za mbegu ya mpunga (Unguja tani 50 na Pemba tani 38) zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima, kwa bei ya ruzuku ya asilimia 50;

c. Jumla ya tani 50 za mbolea (ya kupandia tani 30 na kukuzia tani 20) zimepokelewa kutoka Kampuni ya 'Minjingu Mines and Fertilizers Ltd' na imesambazwa kwa wakulima Unguja na Pemba;

d. Kukamilika kwa ujenzi wa ghala la kuhifadhia chakula lililopo Kizimbani Unguja lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,500 za nafaka;

e. Kuzinduliwa kwa Hifadhi Hai ya Jozani na Ghuba ya Chwaka ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman, hatua itakayochochea kuongezeka kwa idadi ya wageni na ukusanyaji wa mapato;

f. Jumla ya watalii 63,659 walitembelea Hifadhi za Masingini, Kiwengwa-Pongwe, Jozani na Ngezi kati ya watalii 100,000 waliolengwa ambapo sawa na asilimia 64 ya lengo. Aidha, TZS bilioni 1.097 na Dola za Marekani elfu 75.743 zilikusanywa ikiwa ni viingilio vya utalii;

g. Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya utafiti na tathmini ya kuku;

h. Kuanza kazi ya kupima afya ya udongo Zanzibar ili kujua mahitaji ya virutubisho katika uzalishaji wa mazao ya kilimo yenye tija;

i. Kuadhimishwa kwa maonesho ya Nane Nane – Dole Unguja na Siku ya Chakula Duniani – Chamanangwe Pemba, ambapo wadau wamepatiwa uelewa wa mbinu mbali mbali za ukuzaji wa sekta ya kilimo;

j. Kukamilisha taratibu za kushajiisha uwekezaji wa wazawa katika sekta ya mifugo, hasa kuku wa nyama na mayai na kumpatia mwekezaji wa ndani shamba la Pangeni ambalo linatumika kwa kuendeleza mifugo;

k. Kufanikiwa kwa kampeni ya unywaji wa maziwa mashuleni Unguja na Pemba katika kuimarisha afya na lishe bora ili kuepukana na athari za utapia mlo, udumavu na ukondefu; na

l. Kukamilika kwa Utafiti wa malisho ya majani aina ya JUNCAO ambapo wafugaji 17 wamepatiwa mbegu kwa ajili ya kuzalisha.

**20. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana Wizara yangu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

a. Pamoja na jitihada kubwa za Serikali katika kupambana na changamoto ya wizi wa mazao na mifugo, bado matukio haya yanaendelea kujitokeza. Changamoto zaidi inatokana na kuibuka kwa mifumo ya kuhalalisha wizi huo kwa kuwepo kwa madalali ambao hununua bidhaa za wizi na kuzifikisha sokoni bila kufahamika;

b. Upungufu wa wataalamu wa kada za kilimo, mifugo na maliasili unaotokana na wimbi kubwa la wataalamu kustaafu au kuhamishiwa sekta nyengine wakiwemo mabibi na mabwana shamba;

c. Uvamizi wa maeneo ya kilimo unaosababishwa na ongezeko kubwa la ujenzi wa makaazi na shughuli nyengine za kimaendeleo;

d. Uwepo wa bei kubwa ya pembejeo za kilimo;

e. Kuendelea kwa athari ya mabadiliko ya tabianchi kunakopelekea uhaba wa mvua, maradhi katika mazao na upungufu wa malisho kwa mifugo;

f. Kuendelea kwa uharibifu wa misitu unaotokana na shughuli za kibinadamu kama vile uvunaji wa asali kwa kutumia njia za kienyeji; na

g. Upungufu wa vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri, ofisi za Wilaya na vifaa vya ofisi.

**21. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Wizara imechukua hatua zifuatazo:

a. Kuangalia upya taratibu za udhibiti wa mazao na mifugo mashambani kabla ya kuyasafirisha kuelekea sokoni. Tunaomba vyombo husika viendeleze jitihada za kutatua changamoto ya wizi wa mazao na mifugo;

b. Kuwasilisha mapendekezo ya uajiri Ofisi Kuu ya Utumishi Serikalini;

c. Kuendelea kufanya mapitio ya Sera ya Sekta ya Kilimo ili kuhakikisha maeneo ya kilimo yanayomilikiwa na Wizara na wananchi yanapatiwa hatimiliki na yanatumika kwa shughuli za kilimo;

d. Kushirikiana na Wizara ya Kilimo Tanzania Bara katika kuratibu na kuandaa mfumo wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa njia ya kidijitali; na

e. Kuendelea kufanya tafiti juu ya mazao ya kilimo na mifugo yanayohimili athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuhamasisha wananchi kulima na kufuga.

**Fedha Iliyopatikana kwa Kipindi cha Utekelezaji**

22. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, iliidhinishiwa kutumia TZS bilioni 53.590 kati ya fedha hizo TZS bilioni 23.248 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 11.887 kwa Mishahara na TZS bilioni 4.765 kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni 6.596 ikiwa ni Ruzuku (TZS bilioni 3.645 kwa Mishahara na TZS bilioni 2.951 kwa matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

23. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara iliombewa TZS bilioni 30.341 (TZS bilioni 21.647 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS bilioni 8.694 kutoka SMZ).

24. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara imepata TZS bilioni 32.747 sawa na wastani wa asilimia 61 ya fedha zilizoidhinishwa, kati ya hizo TZS bilioni 14.159 zimetumika kwa matumizi ya kawaida (TZS bilioni 12.657 kwa mishahara na TZS bilioni 1.502 kwa matumizi mengineyo). Aidha, ruzuku ya TZS bilioni 5.987 (TZS bilioni 5.093 kwa mishahara na TZS milioni 894 kwa matumizi mengineyo) ilipatikana kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Machi, 2023 Wizara imepata TZS bilioni 12.601 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (Kiambatanisho Nam. 6).

**UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023.**

25. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo imesimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021 - 2026 na Mipango Mkakati ya Kisekta ikiwemo Mpango wa Maendeleo ya Sekta wa Kilimo. Utekelezaji wa Mikakati hii umesaidia kuongezeka kwa taaluma na teknolojia kwa wakulima hasa wa mazao ya mboga, matunda na viungo jambo lililopelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hayo.

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kutekeleza programu kuu nne na Miradi sita ya Maendeleo. Programu hizo ni kama ifuatavyo:

1) Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
2) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;
3) Programu ya Maendeleo ya Mifugo; na
4) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

Aidha, Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa ni ifuatayo;-

1) Mradi wa Kudhibiti Nzi wa Matunda;
2) Mradi wa Kupunguza Athari za Upotevu wa Mazao;
3) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji;
4) Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania;
5) Mradi wa Kurejesha Urithi wa Kijani; na
6) Mradi wa kuendeleza Miundombinu ya Mifugo.

27. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ilikusudia kutekeleza shughuli zifuatazo:

1. Kujenga miundombinu ya umwagiliaji hekta 370 na kuunga umeme wa njia kubwa bonde la Cheju 'B';

2. Kuendelea kuhamasisha kilimo biashara katika mazao ya mboga, matunda na viungo kwa kutumia teknolojia za kisasa, ili kuongeza uzalishaji wenye tija na uhifadhi wa mazingira;

3. Kuanzisha miradi midogo itakayopelekea kuongeza kipato kwa Wakala wa Matrekta ikiwemo; kituo cha mafunzo ya udereva, eneo la kuoshea magari na kutengeneza zana ndogo za kilimo na kuziuza kwa wakulima;
4. Kukamilisha ujenzi wa maghala mawili (2) ya hifadhi ya chakula yatakayohifadhi jumla ya tani 2500;
5. Kupanda miti hekta 130 (hekta 100 Mashamba ya Serikali na 30 Mikoko), na kuhamasisha jamii kupanda hekta 300 na kutoa huduma kwa mashamba ya Serikali;
6. Kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi kufikia 100,000 kupitia miradi ya uwekezaji katika Hifadhi za Misitu;
7. Kutoa chanjo ya maradhi ya miripuko kwa ng'ombe 30,000; kuku 200,000 na mbwa 8,000 pamoja na kupandisha ng'ombe 2,000 kwa njia ya sindano;
8. Kuimarisha huduma za ugani kwa kuwapatia ushauri wafugaji 13,000 Unguja na Pemba;
9. Kufanya tafiti saba mpya (4 Unguja na 3 Pemba) na kuendeleza tafiti sita (4 Unguja na 2 Pemba) za kilimo na maliasili; pamoja na tafiti za kutatua changamoto za kijamii mbili na kuimarisha miundombinu ya utafiti;
10. Kuendelea na utoaji wa maslahi ya wafanyakazi 1,050 ikiwemo ubani (120) likizo (860), muda wa ziada (60) na kusaidia matibabu (10);
11. Kukamilisha mapitio ya Sheria 2 (Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Mifugo Nam. 11 ya 1999 na Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu Nam. 10 ya 1996);
12. Kutayarisha Mpango Mkakati wa Uzalishaji wa Mifugo, Mkakati wa kuimarisha zao la karafuu na uzalishaji wa mazao ya Viungo nchini, pamoja na kukamilisha Mipango ya Sekta ya Kilimo ya Kiwilaya; na
13. Kusimamia na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa Takwimu za Sekta ya Kilimo.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO

**28. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu ndogo nne zifuatazo:

i. Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji;

ii. Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula;
iii. Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo; na
iv. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI

**Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji**

**29. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Uungaji wa umeme wa njia kuu (3-phase) kwa visima 15 katika bonde la Kilombero pamoja na kumalizia uungaji wa umeme huo katika visima 6 vya bonde la Kibokwa;

b. Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika bonde la Cheju 'A', Kinyasini na Mlemele ambapo jumla ya wakulima 4,475 wanaendelea na shughuli za kilimo cha umwagiliaji maji;

c. Uwekaji sawa wa konde, ujengaji wa misingi ya umwagiliaji maji (irrigation canals) pamoja na misingi ya kutolea maji ya ziada (drainage canals) katika bonde la Mlemele;

d. Kutoa mafunzo kwa wakulima viongozi 200 juu ya usimamizi na utunzaji wa skimu mpya za umwagiliaji maji katika mabonde ya Kinyasini, Cheju na Mlemele; na

e. Kufanya malipo ya fidia kwa wananchi 31 katika bonde la Chaani, Kilombero na Mlemele walioathirika wakati wa utekelezaji wa kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

**30. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 22.103 ambapo TZS bilioni 1.603 kwa kazi za kawaida (TZS bilioni 1.053 Mshahara na TZS milioni 550.482 kwa matumizi mengineyo). Vilevile, programu iliombewa TZS bilioni 20.500 kwa kazi za maendeleo ambapo TZS bilioni 20.000 kutoka kwa wahisani EXIM BANK ya Korea na TZS milioni 500.000 kutoka SMZ. Hadi kufikia Machi, 2023 Programu hii imepata TZS bilioni 12.631. Kati ya fedha hizo TZS bilioni 1.076 kwa Mishahara na TZS milioni 107.875 kwa matumizi mengineyo na TZS bilioni 11.447 kwa kazi za maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.**

**31. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Ekari 28,995 zilizolimwa mpunga (2021/2022) kwa msimu wa vuli na masika zimefanyiwa tathmini ya uzalishaji na mavuno na matokeo yake yameonesha kuwa uzalishaji umepungua kutoka tani 30,353 mwaka 2021 hadi tani 27,947 mwaka 2022;

b. Jumla ya miche 252,404 imeoteshwa ikiwemo 196,370 ya mikarafuu (51,050 Unguja na 145,320 Pemba), 47,992 miti ya matunda (21,236 Unguja na 26,756 Pemba) na 8,042 ya minazi ( 5,000 Unguja 3,042 Pemba);

c. Mitego 8,088 ya kunasia nzi wa matunda (Unguja 4,638 na Pemba 3,450) pamoja na dawa ya kunasia nzi hao lita 700 imesambazwa kwa wakulima;

d. Jumla ya tani 73,339 za mazao mbalimbali zimekaguliwa kwa lengo la kudhibiti maradhi na wadudu waharibifu wa mazao. Aidha, miche ya mazao 1,506 imekaguliwa wakati wa kuingizwa au kusafirishwa nje ya Zanzibar;

e. Jumla ya mabibi na mabwanashamba 42 wamepatiwa mafunzo ya kilimo hai, ukusanyaji wa takwimu na utibabu wa mimea. Aidha, maafisa lishe 56 walipatiwa mafunzo juu ya Muongozo wa Ulaji wa Chakula Zanzibar; na

f. Kitini kinachohusiana na udhibiti wa nzi wa matunda kilitengenezwa na kusambazwa kwa wakulima.

**32. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 11.983 ambapo TZS bilioni 4.754 kwa kazi za kawaida (TZS bilioni 3.429 kwa Mshahara na TZS bilioni 1.325 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2023 Programu hii imepata TZS bilioni 4.614 (TZS bilioni 3.036 ni Mishahara na TZS milioni 425.057 kwa matumizi mengineyo), kwa fedha za Maendeleo zilizopatikana ni TZS milioni 1.153 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo**

**33. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Kuendeleza utoaji wa huduma za matengenezo ya matrekta na zana za kilimo za Serikali na sekta binafsi pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa vifaa vya kazi, vipuri na vilainishaji ambapo matrekta 32 yamefanyiwa matengenezo madogo na yanaendelea kutoa huduma. Vile vile majembe 23 ya kuchimbia, 20 ya kuburugia na 5 ya kuchavangia yamefanyiwa

matengenezo. Aidha, jumla ya ekari 3,542.25 zimechimbwa na ekari 797 zimeburugwa Unguja na Pemba kati ya ekari 10,000 zilizolengwa ambapo ni sawa na asilimia 33 ya lengo; na

b. Maandalizi ya uanzishwaji wa Chuo cha Mafunzo ya Amali katika fani za Matumizi ya zana za Kilimo (*Agromechanization*), Ufundi magari na mashine (*Mechanics*), Uchomeaji vyuma (*Welding*), Uchongaji wa vipuri (*Fiting and Turning*) yameanza ambapo Mamlaka ya Mafuzo ya Amali tayari imefanya ukaguzi wa awali kujionea mazingira, miundombinu na vifaa vya kufundishia. Aidha, kutokana na ukaguzi huo Wakala inaendelea kurekebisha mapungufu yaliyobainika ili kuweza kuendelea na hatua zinazofuata;

**34. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu Ndogo hii iliidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni 2.464 (TZS milioni 846.500 kwa Mshahara na TZS bilioni 1.617 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2023 Programu hii imepata TZS bilioni 1.466 ambapo (TZS milioni 922.914 kwa ajili ya Mishahara na TZS milioni 543.082 kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 60 ya fedha zilizoidhinishwa.

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI**

**35. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Utafiti wa mbegu za mpunga zitakazostahamili maradhi ya ukungu, umanjano na hali ya chumvi umeendelea kwenye maeneo ya majaribio ya Kibondemzungu na Bumbwisudi. Aidha, aina za mbegu 225 kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mpunga (IRRI) ziliendelea na uchunguzi kwa hatua mbali mbali na kwa vigezo maalum vya kisayansi vilivyowekwa. Mbegu ya SUPA BC kilogramu 225 zimevunwa katika eneo la nusu eka ili ipandwe tena kwa eneo kubwa zaidi na hatimae mbegu zitazopatikana zianze kusambazwa kwa wakulima;

b. Kuendelea kusimamia ukuaji wa migomba 200 ya 'Tissue Culture' iliyohamishiwa shambani katika eneo la ZARI na ile iliyopewa baadhi ya wakulima;

c. Utafiti wa matumizi ya mwani kuwa mbolea ya migomba umeendelea kwa kufanya uchunguzi wa udongo, mwani na upandaji wa miche;

d. Kujenga Kitalu nyumba (Screen house) kimoja; na

e. Wafanyakazi tisa wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na saba mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Stashahada (2), Shahada (3) na Shahada ya Uzamili (2).

**36. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni 2.767 (TZS bilioni 2.167 kwa Mshahara na TZS milioni 600.200 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2023 Programu hii imepata TZS bilioni 3.370 (TZS bilioni 3.211 kwa Mishahara na TZS milioni 158.675 kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 121 kwa fedha iliyoidhinishwa. Hali hii ya kuongezeka kwa asilimia ya lengo imetokana na ongezeko la mshahara kutokana na Muundo mpya wa Taasisi.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

**37. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu hii katika Programu Ndogo ya Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu kwa Mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Jumla ya miche 418,617 imeoteshwa (298,600 Unguja na 120,017 Pemba) Kati ya hiyo miche 187,795 ya misitu na miche 110,805 ya matunda na viungo imeoteshwa Unguja. Aidha, Miche 57,900 ya misitu na 62,117 ya matunda na viungo imeoteshwa Pemba;

b. Hekta 45 (32.1 Chaani, 5 Dunga, 5 Kibele na 2.9 Maziwa Ng'ombe) zilipandwa miti katika mashamba ya Serikali kati ya hetka 100 zilizolengwa ambapo ni sawa na asilimia 45. Aidha, hekta 93.3 zimepandwa mikoko (Ha 12 Unguja na Ha 81.3 Pemba) katika Shehia za Unguja Ukuu, Bumbwini, Uzi na Fujoni kwa Unguja; Pia Shehia za Chambani, Kinoe, Tumbe Magharibi, Michenzani, Mtemani, Fundo, Gando, Kisiwa Panza, Kukuu, Pujini, Ndagoni, Makangale, Msuka mashariki, Dodo, Kisiwani, Makoongwe na Sizini kwa Pemba, kupitia miradi ya TASAF;

c. Misitu mitano ya jamii iliopo Wilaya ya Kusini Unguja imefanyiwa tathmini ya hali ya uhuikaji ambapo matokeo yanaonesha kuwa eneo kubwa la misitu hiyo limevamiwa kwa shughuli za kilimo, makaazi na uwekezaji wa miradi ya wawekezaji. Hata hivyo, Rasimu za Mikataba mitatu Mipya zimeandaliwa;

d. Mipaka ya msitu wa hifadhi wa Kiwengwa-Pongwe imehakikiwa katika maeneo ya Kumba Urembo, Mafarasi, Melia na Jomba na imebainika uwepo wa uvamizi wa hifadhi kwa ujenzi wa nyumba za makaazi ya

kudumu pamoja na uwepo wa uzio wa kulinda eneo kwa ajili ya matumizi ya baadae katika eneo la mkabala na Hoteli ya Melia;

e. Kwa kushirikiana na Shirika la Uhifadhi wa Wanyama na Mimea, Wizara inaendelea na tathmini ya bioanuai zilizopo katika Msitu wa Kidikotundu-Nongwe-Vundwe unaotarajiwa kupandishwa hadhi;

f. Jumla ya Miradi mitano (5) ya wawekezaji imepokelewa kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo ya hifadhi za Misitu ikiwemo Jozani, Kiwengwa, Masingini na Ngezi;

g. Uzinduzi wa Hifadhi Hai ya Jozani na Ghuba ya Chwaka umefanyika; na

h. Jumla ya Doria 309 (197 Unguja na 112 Pemba) zimefanyika katika maeneo ya rasilimali za Misitu ambapo matukio 82 (46 Unguja na 36 Pemba) yaliripotiwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu hii iliidhinishiwa TZS bilioni 4.059 (TZS bilioni 2.459 kwa mishahara na TZS milioni 600.664 kwa matumizi mengineyo). Vilevile, Programu hii iliidhinishiwa TZS bilioni 1.000 kwa ajili ya Mradi wa Uhifadhi wa miti ya asili na adimu inayotoweka. Hadi kufikia Machi, 2023 Programu hii imepata TZS bilioni 1.934 ambapo TZS bilioni 1.844 kwa mishahara na TZS milioni 90.261 kwa matumizi mengineyo.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

**39. Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina Programu Ndogo mbili za Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo, pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI).

### Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo

**40. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo kwa Mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Jumla ya ng'ombe 1,091 wamepandishwa kwa njia ya sindano (Unguja 644 na Pemba 447);

b. Katika kuimarisha mbegu bora za malisho kwa ajili ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, jumla ya eka 3 zimepandwa malisho aina ya Juncao grass na Guatamala grass katika shamba la malisho Kizimbani – Unguja;

c. Ili kuimarisha ufugaji bora wa ng'ombe, mbuzi na kuku wa nyama wenye tija, jumla ya wafugaji 156 wa ng'ombe wa maziwa wa Pemba na wafugaji wa kuku 31 wa Unguja wamepewa mafunzo ya ufugaji bora;

d. Wafugaji 17,800 (7,720 Unguja na 10,080 Pemba) wametembelewa na kupewa ushauri juu ya ufugaji bora wa kisasa wenye kuleta tija kwa wafugaji.

e. Jumla ya mbwa 6,633 (4,946 Unguja na 1,687 Pemba) wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa;

f. Kuku 78,833 (70,439 Unguja na 8,394 Pemba) wamechanjwa dhidi ya magonjwa ya kuku wakiwemo kuku 51,855 waliochanjwa dhidi ya ugonjwa wa mahepe (New Castle Disease), kuku 15,355 dhidi ya ugonjwa wa Gumboro, kuku 9,984 ugonjwa wa ndui (Fowl Pox) na kuku 1,637 dhidi ya ugonjwa wa mareck's;

g. Jumla ya ng'ombe 1,965 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu (Black Quarter) na kimeta (Anthrax), ugonjwa wa miguu na midomo (Foot Mouth Disease) na ugonjwa wa ngozi (Lumpy Skin Disease);

h. Sampuli 650 (539 Unguja na 111 Pemba) zilichunguzwa maradhi mbalimbali katika maabara, sampuli 215 ndizo zilizoonekana na vimelea vya maradhi kama vile minyoo (Fasciola & Nematodes), kuharisha damu (Coccidiosis), kichaa cha mbwa (Rabies), ndigana moto (East Coast Fever), ugonjwa wa kukojoa damu (Babesiosis), ugonjwa wa kiwele (Mastitis) na sampuli hizo zimechunguzwa kwenye kinyesi, ubongo, damu na maziwa;

i. Wanyama 358 (mbwa 55 na paka 303) wamefungwa kizazi ili kupunguza idadi ya mbwa na paka wazururaji.

**41. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 7.907 (TZS bilioni 2.157 kwa mishahara na TZS milioni 749.398 kwa matumizi mengineyo). Vilevile, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 5.000 kwa ajili ya Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo. Hadi kufikia Machi, 2023 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni 2.174, sawa na asilimia 27 ya fedha zilizoidhinishwa, ambapo TZS bilioni 2.047 kwa mishahara na TZS milioni 126.803 kwa matumizi mengineyo.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI**

**42. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Uendelezaji wa tafiti tatu zikiwemo tafiti tatu mpya zinazohusiana na (i) Tathmini ya usafi wa Maziwa kwa wafugaji, (ii) Tathmini ya Ufanisi wa Malisho na (iii) Tathmini ya Kuku wa Nyama wanaochinjwa katika umri tofauti;

b. Uendelezaji wa mashamba ya malisho ekari 10 (Chamanangwe 6 na Kizimbani 4);

c. Utayarishaji wa kanuni za Utafiti; na

d. Ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya Taasisi Kizimbani ikiwemo (Ofisi, Banda la Utafiti wa ng'ombe, banda la mbuzi, Ukarabati wa Maabara, jengo la kiwanda cha chakula cha Mifugo na Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano).

**43. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa ruzuku ya jumla ya TZS bilioni 1.365 (TZS milioni 631.300 kwa mishahara na TZS milioni 733.300 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2023 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni 1.150, sawa na asilimia 84 ya fedha zilizoidhinishwa, (TZS milioni 958.504 kwa mishahara na TZS milioni 192.409 kwa matumizi mengineyo).

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO**

**44. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo tatu ambazo ni:

i. Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo;
ii. Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo; na
iii. Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba.

**Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo**

**45. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Wafanyakazi 1,073 wamepatiwa stahiki zao ikiwemo ubani (124) likizo (880) na muda wa ziada (69);

b. Jumla ya wafanyakazi thelathini (30) walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi; na

c. Kuendeleza kazi za uendeshaji na utumishi kwa ujumla.

**46. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu Ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya TZS bilioni 3.216 (TZS bilioni 2.102 kwa mshahara na TZS bilioni 1.113 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2023 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni 1.552 (TZS bilioni 1.302 kwa mishahara na TZS milioni 249.531 kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 48 ya fedha zilizoidhinishiwa.

**Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo**

**47. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Mifugo Nam. 11 ya 1999 yamekamilika na yapo katika hatua ya kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, Mpango Mkakati wa Mboga na Matunda, pamoja na Mpango Mkakati wa Kilimo Hai imekamilishwa na ipo katika hatua za uchapishaji;

b. Tafiti mbili za kiuchumi na kijamii zimefanywa kwa mujibu wa Ajenda ya utafiti ya Zanzibar na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo;

c. Uratibu wa utekelezaji wa Miradi na progarmu za AGRI-CONNECT, TANIPAC, BEVAC, na KILIMO TIJA umefanyika;

d. Mapitio ya utaratibu wa ukusanyaji wa takwimu za kilimo pamoja na changamoto zinazokabili yamefanyika. Maandalizi ya mfumo bora wa ukusanyaji wa takwimu yamefanyika kwa kutoa mafunzo kwa wakusanya takwimu wa kila Wilaya Unguja na Pemba pamoja na kuandaa vitendea kazi. Aidha, rasimu ya kitini cha muhtasari wa takwimu za kilimo imeandaliwa; na

e. Mikutano sita (6) ya ushirikiano katika sekta za kilimo, mifugo na maliasili za SMZ na SMT imefanyika kwa kupishana kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

**48. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu Ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 2.955 (TZS milioni 685.301 kwa mishahara na TZS milioni 425.482 kwa matumizi mengineyo). Aidha, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 1.844 fedha za Maendeleo kutoka SMZ kwa ajili ya Mradi wa Kudhibiti Upotevu wa Mazao. Hadi kufikia Machi, 2023 Programu Ndogo hii imepata TZS milioni 376.754 (TZS milioni 228.642 kwa mishahara na TZS milioni 148.111 kwa matumizi mengineyo).

**Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba**

**49. Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo:

a. Kuratibu vikao na ziara za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;

b. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, vituoni na mashambani;

c. Kuratibu ziara za wageni na viongozi pamoja na kuhudhuria katika vikao, sherehe na kumbukumbu za kitaifa; na

d. Kutatua changamoto za wadau pamoja na kuimarisha mashirikiano na taasisi nyengine (za Serikali, Sekta binafsi, na Taasisi za Kijamii).

**50. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu Ndogo hii iliidhinishiwa TZS bilioni 5.216 (TZS bilioni 3.973 kwa mishahara na TZS bilioni 1.243 kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2023 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni 3.475, sawa na asilimia 66 ya fedha zilizoidhinishwa, (TZS bilioni 3.121 kwa mishahara na TZS milioni 353.889 kwa matumizi mengineyo).

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

**Makadirio ya Mapato**

**51. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, imekadiriwa kukusanya mapato ya TZS bilioni 5.534 kupitia vianzio vyake 11 viliopo Unguja na Pemba (Kiambatanisho Nam. 7A).

**Makadirio ya Matumizi 2023/2024**

**52. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, inaomba kuidhinishiwa kutumia TZS bilioni 98.716, kati ya fedha hizo TZS bilioni 20.461 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 16.887 kwa Mishahara na TZS bilioni 3.574 kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni 9.731 ikiwa ni Ruzuku (TZS bilioni 8.301 kwa Mishahara na TZS bilioni 1.430 kwa matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo (Kiambatanisho Nam. 7B).

**53. Mheshimiwa Spika,** kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Wizara inaombewa jumla ya TZS bilioni 68.524 (TZS bilioni 43.524 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS bilioni 25.000 kutoka SMZ) (Kiambatanisho Nam. 8A, 8B, 8C, 8D, 8E, 8F, 8G na 8H)**.**

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO**

**54. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Kilimo ina Programu zifuatazo:

i. Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
ii. Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;
iii. Programu ya Maendeleo ya Mifugo; na
iv. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

**55. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo inaombewa TZS bilioni 80.541, kati ya hizo TZS bilioni 6.796 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 5.482 Mishahara na TZS bilioni 1.313 kwa matumizi mengineyo). TZS bilioni 7.735 ni Ruzuku (TZS bilioni 6.655 Mshahara na TZS bilioni 1.080 kwa matumizi mengineyo) kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Aidha, programu inaombewa TZS bilioni 66.010 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (TZS bilioni 43.524 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS bilioni 25.000 kutoka SMZ).

**MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.**

**56. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Wizara ya Kilimo Uwagiliaji Maliasili na Mifugo itatekeleza Malengo yafuatayo:

1. Kusimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Wizara;

2. Kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, maliasili na mifugo ikiwemo utoaji wa elimu, udhibiti wa magonjwa na uwepo wa uhakika wa chakula;

3. Kuendeleza utoaji wa huduma za ukulima na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na ushajiishaji wa sekta binafsi;

4. Kuendeleza na kuimarisha tafiti za kilimo, maliasili na mifugo;

5. Kuimarisha upandaji wa miti kwa kuotesha miche 2,000,000 ya Misitu, Mikarafuu, Minazi, Matunda na Viungo na kutathmini hali ya uhuishaji wa miti iliyopandwa;
6. Kuimarisha usimamizi wa misitu pamoja na kuendeleza uwekezaji wa Miradi yenye tija katika hifadhi za misitu;
7. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi na kuweka mazingira bora ya kazi; na
8. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi, ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za kisekta.

**Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji**

**57. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji itatekeleza shabaha zifuatazo:

1. Kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika eneo lenye ukubwa wa hekta 300 katika bonde la Cheju 'B', uungaji wa umeme mkubwa kwenye visima vya umwagiliaji kwenye bonde hilo; sambamba na ujengaji wa misingi ya ndani ya saruji kwenye mabonde mapya sita (Cheju, Kilombero, Kibokwa, Chaani, Kinyasini na Mlemele) ya mradi;
2. Kusimamia maeneo yaliyojengwa miundombinu mipya ya umwagiliaji maji yenye ukubwa wa hekta 1,053 sambamba na maeneo mengine ya zamani kwa kushirikiana na wananchi.
3. Kulipa fidia kwa wananchi wataoathirika na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

**58. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo hii inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni 33.584, kati ya hizo TZS bilioni 1.882 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 1.470 Mishahara na TZS milioni 412.800 kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni 31.201 kwa ajili ya Miradi kutoka Washirika wa Maendeleo na TZS millioni 500 kutoka SMZ.

**Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika Chakula**

**59. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Programu ndogo ya Kilimo na Uhakika Chakula itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kununua mbegu mama ya mpunga tani 8, kuzalisha na kuisambaza kwa wakulima wazalishaji wa mbegu (tani 4 Unguja na tani 4 Pemba);

2. Kufanya mapitio ya mahitaji ya pembejeo nchini kwa mwaka;
3. Kufuatilia uzalishaji wa mpunga katika eneo la ekari 33,800 (20,800 Pemba na Unguja 13,000);
4. Kuotesha miche 1,000,000 (400,000 mikarafuu, 300,000 minazi na 300,000 matunda na viungo);
5. Kununua lita 207 za dawa ya kunasia na kuulia nzi wa matunda;
6. Kuandaa aina nne za vitini kwa ajili ya kutoa taaluma juu ya mbinu bora za uzalishaji wa minazi, mazao ya viungo, matumizi bora ya pembejeo, nzi wa matunda na viwavi vamizi;
7. Kununua mpunga tani 500 kwa ajili ya akiba ya chakula;
8. Kutoa mafunzo ya uhakika wa chakula ikiwemo elimu ya Mfumo wa Ulaji; na
9. Kufanya tathmini ya mwenendo wa hali ya chakula nchini.

**60. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo ya Kilimo na Uhakika wa Chakula inaomba kuidhinishiwa jumla ya TZS bilioni 39.222, kati ya hizo TZS bilioni 4.913 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 4.013 Mishahara na TZS milioni 900 kwa matumizi mengineyo). Aidha, programu inaombewa TZS bilioni 34.309 kwa miradi ya maendeleo (TZS billion 22.500 kutoka SMZ na TZS bilioni 11.809 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar**

**61. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo itatekeleza shabaha zifuatazo:

1. Kuendelea na tafiti 11 na kufanya tafiti mpya tano (5) za kilimo na maliasili;
2. Kuimarisha miundombinu ya utafiti ikiwemo kukarabati baadhi ya majengo na kuendeleza ujenzi wa ofisi ya shamba la viungo Kizimbani;
3. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi kwa kufanya mafunzo ya muda mrefu au mfupi kwa wafanyakazi; na

4. Kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi ikiwemo ununuzi wa vifaa na huduma za kiofisi.

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar inaomba kuidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni 5.352, kati ya hizo (TZS bilioni 4.953 Mishahara na TZS million 400 kwa matumizi mengineyo).

**Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo**

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo itatekeleza shabaha zake kama zifuatazo:

1. Kuendeleza utoaji wa huduma za Matrekta na zana za Kilimo za Serikali, pamoja na kuhakikisha kuwepo vifaa vya kazi, vipuri na vilainishi; na
2. Kuhamasisha sekta binafsi katika kuekeza utoaji wa huduma za Matrekta na zana za kilimo.

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inaomba kuidhinishiwa ruzuku ya jumla ya TZS bilioni 2.383, kati ya hizo (TZS bilioni 1.702 Mishahara na TZS millioni 680.100 kwa matumizi mengineyo).

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU**

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi kutoka 64,000 hadi kufikia 100,000 pamoja na kupitia miradi ya uwekezaji iliyoombwa kuwekeza katika maeneo ya hifadhi za misitu;
2. Kuendelea na taratibu za upandishaji hadhi msitu wa Kidikotundu-Nongwe-Vundwe pamoja na kuanzisha hatua za kupandisha hadhi msitu wa Mtambwe;
3. Kuotesha miche 1,000,000 (800,000 Misitu na 200,000 Matunda na Viungo) na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wahudumu 165 wa vitalu vya miche ya miti;
4. Kuhamasisha upandaji miti hekta 130 (Hekta 100 misitu ya Serikali, na Hekta 30 maeneo ya Mikoko) pamoja na kufanya tathmini ya hali ya uhuikaji;

5. Kuhakiki Mipaka ya mashamba ya Misitu ya Chaani Masingini, Hifadhi ya Kimaumbile Masingini-Dole na Hifadhi ya msitu wa Ufufuma-Pongwe;

6. Kufanya doria 500 katika maeneo ya Misitu ya Hifadhi na Misitu ya Jamii Unguja na Pemba; na

7. Kufanya mapitio ya Sera ya Misitu ya mwaka 1995, pamoja na Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu Nambari 10 ya mwaka 1996.

**66. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni 3.457 kati ya hizo (TZS bilioni 2.512 Mishahara na TZS millioni 430.500 kwa matumizi mengineyo) na TZS milioni 514.000 kwa kazi za maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo**

**67. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kupandisha ng'ombe 2,000 (Unguja 1,200, na Pemba 800) kwa njia ya sindano;

2. Kupanda ekari 10 za malisho aina ya 'JUNCAO' katika shamba la malisho Kizimbani kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mbegu za majani ya malisho ya mifugo;

3. Kutoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kuku kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao, pamoja na mafunzo kwa watoaji wa huduma za msingi vijijini (CAHW'S) 50 ili kuimarisha huduma za mifugo kwa wafugaji;

4. Kuwatembelea wafugaji 15,000 (Unguja 8,000 na Pemba 7,000) na kuwapa ushauri juu ya ufugaji bora wa kisasa wenye kuleta tija kwa wafugaji;

5. Kuchanja kuku 200,000 dhidi ya ugonjwa wa mahepe, gumboro na ndui; Mbwa 8,000 (Unguja 5,000 na Pemba 3,000) dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na Ng'ombe 30,000 dhidi ya magonjwa ya chambavu, kimeta ngozi na miguu na midomo;

6. Kufunga uzazi wanyama 300 (mbwa 50 na paka 250) ili kupunguza tatizo la wanyama wazururaji; na

7. Kuchunguza sampuli 1,200 za maradhi ya mifugo.

**68. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni 5.304 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo (TZS bilioni 2.752 Mishahara na TZS millioni 552.000 kwa matumizi mengineyo). Aidha, inaombewa TZS bilioni 2.000 kwa miradi ya maendeleo kutoka SMZ.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar**

**69. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar itatekeleza shabaha zake kama zifuatazo:

1. Kuendeleza tafiti mbili (2) ikiwemo Tathmini ya Ufanisi wa Malisho na Ufanisi wa Mbuzi wa kienyeji pamoja na machotara wao;
2. Kufanya tafiti tatu mpya ikiwemo tathmini ya usafi wa Maziwa kwa wafugaji, utafiti wa majani ya malisho kwa wafugaji na utafiti wa aina tatu za nyongeza ya chakula (feed additives) kwa kuku wa nyama;
3. Kuendeleza mashamba ya malisho ekari 10 (Chamanangwe 6 na Kizimbani 4); na
4. Kutayarisha Mpango Mkakati na Kanuni za Utafiti wa Mifugo.

**70. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Taasisi ya Utafiti wa Mifugo inaomba kuidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni 1.996 kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 1.646 Mishahara na TZS millioni 350.300 kwa matumizi mengineyo).

**Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo**

**71. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kuendelea na utoaji wa maslahi ya wafanyakazi 389 ikiwemo ubani (177), likizo (144), na muda wa ziada (68);
2. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 35 kwa masomo ya muda mrefu na wafanyakazi 130 kwa masomo ya muda mfupi;
3. Kuwapatia mafunzo ya kujiandaa na kustaafu wafanyakazi 128;

4. Kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali TZS bilioni 5.534; na

5. Kusimamia na kudhibiti mali za Serikali zilizopo Wizarani.

**72. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni 2.441 kwa kazi za kawaida (TZS bilioni 1.733 Mishahara na TZS millioni 707.558 kwa matumizi mengineyo).

**Mipango, Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo**

**73. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi iliyopo chini ya Wizara;

2. Kuimarisha ukusanyaji wa Takwimu za kisekta;

3. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za ndani, Kikanda na Kimataifa; na

4. Kufanya tafiti mbili za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Ajenda ya utafiti wa Zanzibar.

**74. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti inaomba kuidhinishiwa TZS milioni 563.139 kwa kazi za kawaida (TZS milioni 318.889 Mishahara na TZS milioni 244.250 kwa matumizi mengineyo).

**Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba**

**75. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Kilimo Umwagiaji Maliasili na Mifugo - Pemba itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia kazi za kilimo umwagiliaji maliasili na mifugo Pemba.

**76. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za kilimo umwagiliaji maliasili na mifugo Pemba inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni 4.415 kwa kazi za kawaida (TZS bilioni 4.088 Mishahara na TZS millioni 326.792 kwa matumizi mengineyo).

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

77. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya TZS bilioni 5.535 kupitia vyanzo 11 vilivyopo Unguja na Pemba.

78. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, inaomba kuidhinishiwa kutumia TZS bilioni 98.716 ambapo TZS bilioni 20.461 ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni 16.887 kwa Mishahara na TZS bilioni 3.574 kwa matumizi mengineyo). TZS bilioni 9.731 ikiwa ni Ruzuku (TZS bilioni 8.301 Mishahara na TZS bilioni 1.430 matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo (Kiambatisho Nam. 9).

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kutekeleza miradi minane kama inavyoonekana kwenye Kiambatanisho 8A, 8B, 8C, 8D, 8E, 8F, 8G na 8H. Utekelezaji wa Miradi hiyo inaombewa TZS bilioni 68.524 (TZS bilioni 25.000 kutoka SMZ na TZS bilioni 43.524 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

## SHUKURANI

80. **Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huo, sasa natumia nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili na mifugo; zikiwemo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais; Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, na Utawala Bora, Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, UtumishiOfisi ya Rais - Kazi Uchumi na Uwekezaji, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji Nishati na Madini, Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

81. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani za pekee ziende kwenye Wizara na Taasisi zinazoshabihiana na Wizara ya Kilimo kwa upande wa Tanzania Bara. Wizara na Taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wakala wa Mbegu Tanzania (ASA), CARI, Uongozi wa Halmashauri ya Mvomero.

82. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuyashukuru Mashirika binafsi ya ndani na nje ya nchi yakiwemo PBZ, CRDB, EQUITY BANK, ZSTC, PDF (VIUNGO Project), TAHA, UWAMWIMA, FEED THE FUTURE - KILIMO TIJA, COSTECH, COMMUNITY FOREST PEMBA, BEVAC, TAFIRI, TALIRI, TPRI, ZAASO na ZSPCA. Tunazishukuru pia nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia kuendeleza sekta hii, zikiwemo Japan, China, Korea ya Kusini, Marekani, UAE, Oman na Uholanzi, kwa kushirikiana na sisi kuendeleza sekta ya Kilimo. Benki ya Dunia, Benki ya Tanzania ya Kilimo, Benki ya Umoja wa nchi za Ulaya - EU kupitia mradi wa AGRI-CONNECT, Maendeleo ya Afrika, ICRAF, IFAD, UNDP, FAO, JICA, USAID, USDA, KOICA, IITA, IRRI, WCS, GARC, PASS, WHO, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Root and Shoot, Solidaridad, Enabel, NMB, Heifer International, Exim Bank ya Korea, FLI ya Ujerumani na World Vegetable Centre.

83. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru viongozi wa Wizara hii ninayoiongoza wakiwemo; Katibu Mkuu – Ndugu Seif Shaaban Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu – Dk. Omar Ali Amir, Ofisa Mdhamini WKUMM, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Wizara na Bodi ya Ushauri Jozani pamoja na watumishi wote kwa juhudi zao, ushirikiano na ushauri walionipatia jambo ambalo limeniwezesha kusimama hapa leo hii kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

Pia, nawapongeza kwa dhati viongozi wa jumuiya za wakulima na wafugaji, wakulima, wafugaji, watunza mazingira na wadau wote wa sekta za kilimo, maliasili na mifugo kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo kwa ajili ya chakula na biashara pamoja na utunzaji wa misitu nchini.

84. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Viongozi Wateule wote wa Serikali wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Masheha, Vikosi vya SMZ na SMT na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa Hotuba hii ya Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo.

**85. Mheshimiwa Spika,** na Waheshimiwa Wajumbe **nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.**




**MHE. SHAMATA SHAAME KHAMIS**
**WAZIRI,**
**WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO,**
**ZANZIBAR**

**VIAMBATANISHO**


**Kiambatanisho Nam. 1A: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2021 - 2022, Zanzibar**

| Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga 2021 - 2022 - Zanzibar | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ZAO** | **2021** | | **2022** | |
| | **Eneo lillilopndwa (ekari)** | **Uzalishaji (tani)** | **Eneo lillilopndwa (ekari)** | **Uzalishaji (tani)** |
| Muhogo | 30,949 | 181,668 | 34,501 | 202,520 |
| Mpunga wa juu | 25,384 | 25,511 | 26,243 | 23,683 |
| Mpunga wa Kumwagilia | 2,789 | 4,842 | 2,843 | 4,265 |
| Migomba | 7,104 | 61,094 | 6,086 | 52,337 |
| V/vikuu | 1,549 | 7,746 | 1,338 | 6,692 |
| Majimbi | 1,148 | 4,386 | 1,009 | 3,852 |
| J/kunde | 2,233 | 1,117 | 2,069 | 1,035 |
| V/Vidogo | 5,259 | 36,813 | 5,755 | 40,286 |
| Mtama | 367 | 139 | 609 | 231 |
| N/nyasa | 775 | 372 | 1,301 | 624 |
| Mahindi | 3,256 | 1,628 | 3,002 | 1,501 |
| Mbaazi | 497 | 1,606 | 663 | 2,142 |
| Uwele | 201 | 40 | 204 | 41 |
| Maboga | 297 | 1,407 | 592 | 2,807 |
| Chooko | 314 | 126 | 411 | 164 |
| Mboga na matunda | 16,470 | 64,820 | 17,692 | 66,304 |
| **Jumla** | **98,591** | **393,315** | **104,316** | **408,484** |


**Kiambatanisho Nam. 1B: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2021 – 2022**




**Kiambatanisho Nam. 2A: Idadi ya Mifugo iliyokaguliwa na Kuchinjwa, 2022**





**Kiambatanisho Nam. 2B: Idadi ya Kuku waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2022**



**Kiambatanisho Nam. 3: Uzalishaji wa Mayai na Maziwa 2022**




**Kiambatanisho Nam. 4: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu kwa Mwaka 2021 na 2022**



**Kiambatanisho Nam. 5: Upatikanaji wa Mapato Julai 2022 hadi Machi, 2023**

| KASMA NAMBA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2022/2023 | MAKUSANYO HALISI | % |
|---|---|---|---|---|
| **OFISI KUU PEMBA** | | | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 45,561,000 | 35,490,141 | 78 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 1,566,000 | 16,500 | 1 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 150,000,000 | 53,650,000 | 36 |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 28,922,000 | 40,095,296 | 139 |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 14,383,000 | 13,730,100 | 95 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 626,000 | 298,000 | 48 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI NGEZI | 10,438,000 | 8,898,894 | 85 |
| | **JUMLA PEMBA** | **251,496,000** | **152,178,931** | **61** |
| **IDARA YA MISITU** | | | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 293,750,000 | 242,125,028 | 82 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 8,350,000 | 12,307,100 | 147 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI JOZANI | 1,036,366,000 | 1,092,454,104 | 105 |
| | **JUMLA** | **1,338,466,000** | **1,346,886,232** | **101** |
| **IDARA YA KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA** | | | | |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 134,024,000 | 113,574,474 | 85 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 12,000,000 | 2,540,000 | 21 |
| | MAPATO YA MPUNGA | - | 152,083,900 | |
| | **JUMLA** | **146,024,000** | **268,198,374** | **184** |
| **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO** | | | | |
| 1423002 | MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE | 25,000,000 | 12,994,500 | 52 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 90,000,000 | 69,100,000 | 77 |
| 1422066 | ADA YA UINGIZAJI WAGENI | 20,000,000 | 17,328,000 | 87 |
| | **JUMLA** | **135,000,000** | **99,422,500** | **74** |
| **IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO** | | | | |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 2,576,993,000 | 1,667,045,089 | 65 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 599,000 | 2,200,000 | 367 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 6,000,000 | | |
| | **JUMLA** | **2,583,592,000** | **1,669,245,089** | **65** |
| **WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO** | | | | |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA | 245,422,000 | 312,723,019 | 127 |
| | **JUMLA** | **245,422,000** | **312,723,019** | |
| | **JUMLA UNGUJA** | **4,448,504,000** | **3,696,475,214** | **83** |
| | **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | **4,700,000,000** | **3,848,654,145** | **82** |

**Kiambatanisho Nam. 6: Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2022 Hadi Machi, 2023**

| PROGRAM KUU/ PROGRAM NDOGO | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA KIPINDI CHA JULAI HADI MACHI, 2023 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MSHAHARA | MATUMIZI KAWAIDA | RUZUKU MSHAHARA | RUZUKU KAWAIDA | MAENDE LEO SMZ | MAENDELEO MUHISANI | JUMLA |
| **PL0101: Maendeleo ya Kilimo** | **4,112,464,325** | **532,932,993** | **4,134,289,335** | **701,757,000** | **0** | **12,600,898,923** | **22,082,342,576** |
| SL010101: Kuendeleza miundombinu ya Umwagiliaji maji | 1,076,110,870 | 107,875,304 | | | | 11,446,993,736 | 12,630,979,910 |
| SL010102: Utafiti na Mafunzo ya kilimo - ZARI | | | 3,211,375,430 | 158,675,000 | | | 3,370,050,430 |
| SL010103: Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula | 3,036,353,455 | 425,057,689 | | | | 1,153,905,187 | 4,615,316,331 |
| SL010105: Karakana ya Matrekta | | | 922,913,905 | 543,082,000 | | | 1,465,995,905 |
| **PL0102: Maendeleo ya Raisilimali za Misitu** | **1,844,383,385** | **90,261,857** | **0** | **0** | **0** | **0** | **1,934,645,242** |
| SL010201: Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu | 1,844,383,385 | 90,261,857 | | | | | 1,934,645,242 |
| **PL0103: Maendeleo ya Mifugo** | **2,047,835,065** | **126,803,743** | **958,504,440** | **192,409,200** | **0** | **0** | **3,325,552,448** |
| SL010301 Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo | 2,047,835,065 | 126,803,743 | | | | | 2,174,638,808 |
| SL010303: Taasisi ya Utafiti wa Mifugo - ZALIRI | | | 958,504,440 | 192,409,200 | | | 1,150,913,640 |
| **PL0105: Mipango na Usimamizi wa Kilimo Maliasili na Mifugo** | **4,652,600,180** | **751,532,227** | **0** | **0** | **0** | **0** | **5,404,132,407** |
| SL010501: Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 1,302,657,630 | 249,531,580 | | | | | 1,552,189,210 |
| SL010502: Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 228,642,835 | 148,111,647 | | | | | 376,754,482 |
| SL010503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo - Pemba | 3,121,299,715 | 353,889,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3,475,188,715 |
| **JUMLA KUU** | **12,657,282,955** | **1,501,530,820** | **5,092,793,775** | **894,166,200** | **0** | **12,600,898,923** | **32,746,672,673** |

**Kiambatanisho Nam. 7A: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024**

| KASMA NAMBA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2023/2024 |
|---|---|---|
| **OFISI KUU PEMBA** | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 45,561,000 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 1,500,000 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 50,000,000 |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 30,000,000 |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 17,000,000 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 500,000 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI NGEZI | 15,000,000 |
| 1422126 | ADA YA MAZAO YA KILIMO | 548,000 |
| 1422068 | ADAYA MAZAO YA MIFUGO | 500,000 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 30,000,000 |
| **JUMLA PEMBA** | | **190,609,000** |
| **IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA** | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 315,100,000 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 25,000,000 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI JOZANI | 1,217,300,000 |
| | **JUMLA** | **1,557,400,000** |
| **IDARA YA KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA** | | |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 176,000,000 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 15,000,000 |
| 1421001 | MAUZO YA MICHE | 10,000,000 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 65,000,000 |
| | **JUMLA** | **266,000,000** |
| **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO** | | |
| 1423002 | MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE | 15,000,000 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 80,000,000 |
| 1422066 | ADA YA UINGIZAJI WAGENI | 30,000,000 |
| | **JUMLA** | **125,000,000** |
| **IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO** | | |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 2,839,459,000 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 4,500,000 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | - |
| | **JUMLA** | **2,843,959,000** |
| **WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO** | | |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA | 551,880,000 |
| | **JUMLA** | **551,880,000** |
| **JUMLA UNGUJA** | | **5,344,239,000** |
| **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | | **5,534,848,000** |

## Kiambatanisho Nam. 7B: Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024

| MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA PROGRAMU KUU KWA MWAKA 2023/2024, | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Program** | **Makadirio** | **Mshahara** | **Matumizi Mengineyo** | **Ruzuku** | | **Maendeleo** | |
| | | | | **M/Mengineyo** | **Mshahara** | **SMZ** | **Muhisani** |
| **PL0101: Maendeleo ya Kilimo** | **80,541,262,223** | **5,482,955,897** | **1,312,900,000** | **1,080,100,000** | **6,654,900,000** | **23,000,000,000** | **43,010,406,326** |
| SL010101: Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji *(00000P001: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji)* | 33,583,797,894 | 1,470,405,183 | 412,800,000 | | | 500,000,000 | 31,200,592,711 |
| SL010102: Utafiti na Mafunzo ya Kilimo - ZARI | 5,352,500,000 | | | 400,000,000 | 4,952,500,000 | | |
| SL010103: Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula | 4,912,650,714 | 4,012,550,714 | 900,100,000 | | | | |
| *00000P028: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula* | 22,500,000,000 | | | | | 22,500,000,000 | |
| *00000P017: Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC)* | 485,558,000 | | | | | | 485,558,000 |
| *00000P025: Mradi wa Kudhibiti Nzi Waharibifu wa Matunda (Fruit Flies)* | 421,575,615 | | | | | | 421,575,615 |
| *00000P021: Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (Agriconnect)* | 8,562,680,000 | | | | | | 8,562,680,000 |
| *00000P031: Mradi wa Kilimo Tija (USAID)* | 2,340,000,000 | | | | | | 2,340,000,000 |
| SL010105: Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | 2,382,500,000 | | | 680,100,000 | 1,702,400,000 | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PL0102: Maendeleo ya Rasilimali za Misitu** | **3,456,634,822** | **2,512,134,822** | **430,500,000** | | | | **514,000,000** |
| SL010201: Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu | 2,942,634,822 | 2,512,134,822 | 430,500,000 | | | | |
| *00000P030: Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC)* | 514,000,000 | | | | | | 514,000,000 |
| **PL0103: Maendeleo ya Mifugo** | **7,299,980,059** | **2,751,780,059** | **552,000,000** | **350,300,000** | **1,645,900,000** | **2,000,000,000** | |
| SL010301: Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo | 3,303,780,059 | 2,751,780,059 | 552,000,000 | | | | |
| *00000P029: Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo* | 2,000,000,000 | | | | | 2,000,000,000 | |
| SL010303: Taasisi ya Utafiti wa Mifugo | 1,996,200,000 | | | 350,300,000 | 1,645,900,000 | | |
| **PL0105: Mipango na Usimamizi wa Kilimo Maliasili na Mifugo** | **7,418,529,222** | **6,139,929,222** | **1,278,600,000** | | | | |
| SL010501: Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 2,440,885,896 | 1,733,327,896 | 707,558,000 | | | | |
| SL010502: Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 563,139,797 | 318,889,797 | 244,250,000 | | | | |
| SL010503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo - Pemba | 4,414,503,529 | 4,087,711,529 | 326,792,000 | | | | |
| **JUMLA KUU** | **98,716,406,326** | **16,886,800,000** | **3,574,000,000** | **1,430,400,000** | **8,300,800,000** | **25,000,000,000** | **43,524,406,326** |

## Kiambatanisho Nam. 8A: Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliajimaji

| |
|---|
| Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mradi huu ulipangiwa TZS bilioni 20.500 ambapo TZS milioni 500.000 kutoka SMZ na TZS bilioni 20 kutoka EXIM BANK ya Korea. Hadi kufikia Aprili 2022 mradi umepata TZS bilioni 11.447 kutoka EXIM BANK ya Korea. |
| **Malengo kwa Mwaka 2022/2023** |
| i. Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 370 katika bonde la Cheju B pamoja na ujengaji wa misingi ya ndani (Tertiary canals) kwa kiwango cha saruji yenye urefu wa kilomita 47.74 katika bonde la Cheju A, Kinyasini, Kilombero, Kibokwa, Chaani, Cheju na Mlemele;<br>ii. Uungaji wa umeme wa njia kuu (3-phase) kwa visima 15 katika bonde la Cheju B pamoja na kumalizia uungaji wa umeme huo katika bonde la Kibokwa na Kilombero;<br>iii. Uwekaji sawa wa konde katika bonde la Mlemele pamoja na ujengaji wa viungio (structures) katika misingi ya umwagiliaji maji (irrigation canals) pamoja na misingi wa kutolea maji ya ziada (drainage canals);<br>iv. Kufanya ukarabati na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji na kutoa mafunzo kwa wakulima na wataalamu juu ya usimamizi na uendeshaji wa skimu pamoja na kushajiisha wakulima kuchangia gharama; na<br>v. Kufanya malipo ya fidia kwa wananchi watakao athirika wakati wa utekelezaji wa kazi za ujenzi wa miundombinu. |
| **Utekelezaji wa Malengo** |
| i. Kazi za ujenzi na usimamizi wa mradi wa umwagiliaji maji zinaendelea katika mabonde sita kwa Unguja na Pemba, zikijumuisha ukamilikaji wa mabwawa matatu kwa upande wa Unguja (bwawa la Kinyasini na la Chaani) na upande wa Pemba (bwawa la Mlemele) na kuanza kuhifadhi maji ya umwagiliaji ya maeneo hayo. Kwa upande wa bonde la Mlemele kazi ya uwekaji kifusi umekamilika na kunaendelea na kazi ya ujenzi wa viungio (structures) ya misingi ya umwagiliaji maji pamoja na uwekaji sawa wa konde wa mwisho na kwa upande wa bonde la Cheju kazi inayoendelea ni uungaji wa umeme mkubwa kwenye visima na uwekaji wa kifusi chenye urefu wa kilomita 16 kwenye njia za mashambani;<br>ii. Kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ya maji zinaendelea na utekelezaji wake ambao umefikiwa 90%, kwa upande wa asilimia za utekelezaji kwa kila bonde ni kama ifuatavyo; Kilombero hekta 292 imefikia (85%), Mlemele hekta 44 imefikia (90%) na Cheju hekta 314 imefikia (90%);<br>iii. Malipo ya fidia ya mazao ya wakulima yamefanyika kwa jumla ya wakulima 31 katika mabonde ya Chaani, Cheju, Kilombero na Mlemele; na<br>iv. Kazi za Uungaji wa umeme wa njia kuu (3 phase line) katika skimu za umwagiliaji maji zinaendelea ambapo zimeanza katika bonde la Cheju na kufikiwa asilimia 80 kwa utekelezaji wake Cheju na kazi hii itaendelea kwa mabonde ya Kilombero na Kibokwa. |
| **Gharama za mradi:** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mradi huu unaombewa TZS bilioni 31.701 ambapo TZS milioni 500.000 kutoka SMZ na TZS bilioni 31.201 kutoka EXIM BANK ya Korea. |
| **SHABAHA ZA 2023/2024**<br>i. Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 300 katika bonde la Cheju B, Uungaji wa umeme mkubwa kwenye visima vya umwagiliaji maji pamoja na ujengaji wa misingi ya ndani kwa kiwango cha saruji yenye urefu wa kilomita 47.74 katika bonde la Cheju A, Kinyasini, Kilombero, Kibokwa, Chaani na Mlemele;<br>ii. Kusimamia maeneo yaliyojengwa miundombinu mipya ya umwagiliaji maji yenye ukubwa wa hekta 1053 ikiwemo kuwapa mafunzo ya taaluma juu ya kilimo cha umwagiliaji maji kwa kamati na wakulima viongozi sambamba na ukamilishaji wa utatuaji wa changamoto ya uvujaji maji katika bwawa la Chaani na ukamilishaji wa uungaji wa bomba za maji kwenye visima katika bonde la kilombero; na<br>iii. Kuwalipa fidia wananchi wataoathirika na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. |

## Kiambatanisho Nam 8B: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula

| |
|---|
| **Huu ni mradi mpya:** Kwa mwaka 2023/2024 Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 22.500 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - SMZ |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kukarabati maghala na ununuzi wa chakula |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi**<br>i. Kuhakikisha haki ya upatikanaji wa chakula katika ngazi ya kaya na taifa inafikiwa. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Serikali**<br>i. Kukarabati ghala moja la kuhifadhia chakula; na<br>ii. Kununua na kuijengea mitambo ya baridi katika maghala. |

**Kiambatanisho Nam. 8C: Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC)**

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2022/2023:** Kwa mwaka 2022/2023: Mradi uliombewa TZS bilioni 1.259 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**.** |
| **Malengo ya Mwaka 2022/2023** |
| i. Udhamini wa wanafunzi wawili (2) wa shahada ya uzamili na mmoja (1) wa shahada ya uzamivu unaendelea katika vyuo vya Tanzania;<br>ii. Mashine za kupima sumukvu katika bidhaa za chakula zimenunuliwa na kukabidhiwa katika taasisi ya ZARI na ZFDA. Mashine hizo ni HPLC kwa ZFDA na Evidence Investigator kwa ZARI, pia wataalamu katika taasisi hizo wamepatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mashine hizo;<br>iii. Uchunguzi wa hali ya Sumukuvu (Situational Analysis on Aflatoxin) hapa Zanzibar umekamilika na ripoti kamili imewasilishwa katika ofisi ya Mradi kwa utekelezaji;<br>iv. Ghala la kuhifadhia nafaka limekamilika na kukabidhiwa Kizimbani Unguja na Ole Dodeani Pemba ujenzi umefikia asilimia 85;<br>v. Mafunzo ya uelewa na udhibiti wa Sumukuvu kwa wafanyabiashara 200 (Unguja 120 na Pemba 80) yamefanyika;<br>vi. Mafunzo ya siku tatu (3) kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima 30 yametolewa;<br>vii. Mafunzo ya uelewa wa Sumukuvu kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi yamefanyika;<br>viii. Kamati mbili (2) zenye wajumbe kutoka ngazi ya Shehia, Wilaya, Mkoa na Wizara zimeundwa na kuwezeshwa kufanya usimamizi wa maghala Unguja na Pemba;<br>ix. Wawezeshaji wawili kutoka ZFDA na ZBS walihudhuria mafunzo ya wiki moja yaliyowajengea uwezo katika kutoa elimu ya udhibiti wa sumu kuvu; na<br>x. Kwa kushirikiana na VETA na Mamalaka ya Ufundi Stadi Zanzibar VTA mradi unaendelea na usajili wa vijana 40 Unguja na Pemba kupitia Mabaraza ya Vijana ya Wilaya kwa ajili ya kuwapa mafunzo hayo. |
| **Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2022/2023** |
| i. Ghala moja limekabidhiwa na moja lipo 85%;<br>ii. Kutoa vipindi vitatu (3) vya radio; na<br>iii. Kutoa mafunzo kwa mabwana/mabibi shamba 60. |
| **Kwa mwaka 2023/2024:** Mradi unaombewa jumla ya TZS milioni 485.558 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |
| **Malengo kwa mwaka 2023/2024** |
| i. Kuendelea na udhamini wa wanafunzi wa shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu;<br>ii. Kuendelea na malipo ya wakandarasi wa ujenzi wa ghala la Pemba;<br>iii. Kuendelea na shughuli za kutoa elimu ya sumukuvu kwa wadau kwa mfano wakulima;<br>iv. Kushiriki katika maonesho ya kitaifa;<br>v. Kutengeneza vifaa vya uelimishaji wa jamii k.v vipeperushi mabango kofia na fulana;<br>vi. Kununua vifaa kwa ajili ya maghala Unguja na Pemba;<br>vii. Usimamizi na uendeshaji wa ofisi; na<br>viii. Kwa kushirikiana na VETA na Mamalaka ya Ufundi Stadi Zanzibar VTA mradi utaendelea kuwapa mafunzo ya utengenezaji wa vihenge vya chuma kwa vijana 40 Unguja na Pemba. |

## Kiambatanisho Nam. 8D: Mradi wa Kudhibiti Nzi Waharibifu wa Matunda

**Kwa mwaka 2022/2023:** Mradi uliombewa TZS milioni 738.2 (TZS milioni 350 kutoka Serikalini na TZS milioni 388.240 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo IAEA)**.**

**Utekelezaji wa Malengo 2022/2023**

i. Ziara mbili (2) za wataalamu Elekezi wa mifumo ya kunasia nzi wa matunda zimefanyika;
ii. Kusambaza dawa aina ya Atomiki (IAEA) ya kunasia nzi wa matunda Naturalyte Fruit Fly Bait lita 420; na
iii. Kushiriki Kongamano la Kimataifa la Nzi wa Matunda lililofanyika nchini Australia kuanzia tarehe 13-18 Novemba 2022, kwa udhamini wa IAEA.

**Kwa mwaka 2023/2024:** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS milioni 421.575 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (IAEA).

**Malengo kwa mwaka 2023/2024**

**Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Serikali**

i. Kufanya upembuzi yakinifu juu ya matumizi ya mbinu mchanganyiko katika maeneo maalumu;
ii. Kukusanya takwimu za matunda kwa utaratibu maalum (systematic fruit sampling);
iii. Kununua vifaa vya kukusanyia sampuli za wadudu wa matunda;
iv. Kununua vifaa kwa ajili ya kampeni ya nzi wa matunda; na
v. Uendeshaji na Uratibu wa Mradi.

**Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

i. Kununua vifaa vya kuimarisha mfumo wa uingizaji na utoaji wa mazao;
ii. Kununua vifaa vya maabara ya karantini;
iii. Kununua vifaa na dawa za kunasia nzi wa matunda; na
iv. Kufanya ziara za kimafunzo kwa viongozi na watendaji.

## Kiambatanisho Nam. 8E: Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (AGRICONNECT)

Kwa mwaka 2022/2023: Mradi uliombewa TZS bilioni 7.967 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo - Umoja wa Nchi za Ulaya, na ulitumia TZS bilioni 2.433,687.528.64.

**Malengo ya mwaka 2022/2023**

- i. Wakulima wadogo wameongeza utaalamu wa kilimo chao sambamba na kupata soko na taarifa za uzalishaji;
- ii. Kuongeza uwezo wa wasindikaji wadogo na wafanyabiashara kwa kuimarisha na kuwaunganisha baina ya wazalishaji, wasindikaji na wauzaji;
- iii. Wazalishaji wa mboga, viungo na matunda kusogezewa huduma za ki-fedha na za ki-biashara za kisasa ikiwemo za kimtandao;
- iv. Kuongeza mwamko kwa watunga sera kuhusu vikwazo vinavyorudisha nyuma biashara ya mboga, viungo na matunda;
- v. Kujenga uwezo wa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kutayarisha viwango vya mazao ya mboga, viungo na matunda; na
- vi. Kuwajengea uwezo kupata na kutumia vyakula vyenye lishe bora (hasa wanawake) ambavyo vinazingatia mfumo wa kilimo kinachoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

**Utekelezaji wa Malengo ya mwaka 2022/2023**

- i. Kutoa mafunzo kwa wakulima 17,589 juu ya kanuni za kilimo bora cha Mboga na matunda;
- ii. Kutoa mafunzo kwa Wahudumu wa Kujitolea wa Afya (CHV) 132 na kuweza kuwafikia wanajamii 7,566 kuwafundisha elimu ya lishebora kwa wajawazito na watoto chini ya miaka 5;
- iii. Kuunganisha na Masoko: Jumla ya wakulima 242 wameunganishwa na Masoko;
- iv. Kuzindua Kituo cha kutoa Taaluma za Tasnia ya Hoticulture hapo Mpendae;
- v. Kujenga soko na vyumba vya kuhifadhia mazao ya mboga na matunda, Unguja na Pemba. Kununua mashine za kuongeza thamani mazao; na
- vi. Kukamilisha mpango mkakati wa kuendeleza horticulture Zanzibar.

**Kwa mwaka 2023/2024:** Mradi umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 8.563 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo - Umoja wa Nchi za Ulaya

- i. Kuwajengea uwezo wakulima 10,500, hasa wanawake kupata na kutumia vyakula vyenye lishe bora ambavyo vinazingatia mfumo wa kilimo kinachoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi;
- ii. Kuongeza thamani kwa kujenga majengo mawili ya kusindika mazao, kushughulikia masoko na kilimo biashara;
- iii. Kuwajengea uwezo wanawake;
- iv. Kuongeza kipato cha wakulima wadogo 1,767 kwa kuwasogezea huduma za fedha kuendeleza uzalishaji wa mazao ya mboga, viungo na matunda;
- v. Kuwapatia mitaji wajasiriamali na wakulima wadogo vikundi 45 kuendeleza miradi ya kilimo cha horticulture pamoja na usindikaji;
- vi. Kujengea uwezo wakulima kwa utaalamu wa Viwango endelevu vya Hiari (VSS) pamoja na mchakato wa kuwa na vyeti vya uthibitisho wa mazao;
- vii. Kufanya Utafiti wa kudhibiti viumbe waharibifu wa mazao, pamoja na kuchunguza mabaki ya madawa ya mimea katika mazao; na
- viii. Kuendeleza mpango wa kusambaza taarifa za masoko na elimu kwa wadau wa mazao ya bustani.

## Kiambatanisho Nam. 8F: Mradi wa Kilimo Tija

**Huu ni mradi mpya:** Kwa mwaka 2023/2024 Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS Bilioni 2.340 kutoka kwa Washirika wa Maendleo - USAID

**Lengo kuu la Mradi:** Kuendeleza fursa za kiuchumi katika mifumo ya masoko ya mazao ya mboga na matunda, hasa kwa vijana.

**Malengo Makhsusi ya Mradi**

i. Kuimarisha mifumo ya masoko ya mazao ya mboga na matunda kwa kuongeza fusra za ajira na ujasiriamali;
ii. Kuongeza upatikanaji wa teknpolojia za kilimo zinazoimarisha uzalishaji wa kilimo kibiashara na unaozingatia mabadiliko ya tabianchi; na
iii. Kuimarisha mazingira wezeshi ya kuendeleza mifumo ya masoko.

**Kazi zilizopangwa kutekelezwa**

i. Kusaidia shughuli za ugani katika Wizara ya Kilimo ili kuweza kufikisha huduma bora za ugani kwa wakulima kwa kuimarisha uwezo wa mabwana shamba pamoja na kushajiisha wadau zaidi wa ugani;
ii. Kuisaidia Wizara kuanzisha Kanzidata ya wakulima itakayoimarisha ukusanyaji wa taarifa, ukaguzi na kusaidia mipango ya wizara;
iii. Kuhimiza upatikanaji na matumizi ya teknolojia za kilimo zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi na kuongeza tija ili kuhakikisha kuwepo kwa uzalisjhaji wa mazao mwaka mzima huku ikisaidia wakulima kufikia masoko;
iv. Kuongeza jitihada katika kuimarisha mabaraza ya vijana katika ngazi ya wilaya ili kuwajenga uwezo katika uzalishaji wa mazao ya kilimo pamoja na kuendeleza biashara katika minyororo ya thamani;
v. Kusaidia jitihada za sekta binafsi katika kuwawezesha wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani kufikia mitaji itakayosaidia biashara zao;
vi. Kuisaidia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI kuandaa benki ya hifadhi ya mimea mazao kwa mazao ya mboga na matunda yenye asili ya Afrika;
vii. Kushirikiana na sekta binafsi katika kusaidia kuandaa ramani ya udongo ya Zanzibar;
viii. Kushajiisha mashirikiano baina ya ZARI na sekta binafsi kuanzisha vitalu kwa ajili ya kufanyia majaribio na usambazaji wa matokeo ya majaribio ya mbegu bora za mimea;
ix. Kusaidia kuimarisha vikundi vya ushirika vya mboga na matunda Zanzibar katika maeneo ya uzalishaji, utawala bora na upatikanaji wa mitaji;
x. Kuwajenga uwezo watendaji wanaosimamia sera na mipango katika kufanya shughuli za ufuatiliaji na tathmini; na
xi. Kusaidia maandalizi ya mafunzo endelevu ya kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno.

## Kiambatanisho Nam. 8G: Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC)

| |
|---|
| Mradi huu unatekelezwa kisiwani Pemba na Shirika la Maendeleo la Ubeligiji (Enabel) chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya. Kwa mwaka fedha 2022/2023 mradi huu ulitengewa TZS milioni 514.000. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuimarisha mchango wa sekta ya ufugaji nyuki katika ukuaji wa uchumi shirikishi nchini Tanzania |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:** Kuiwezesha asali bora inayozalishwa kwa njia endelevu ya mazingira kupenya katika masoko. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa**<br>i. Kutoa mafunzo kwa wafugaji nyuki;<br>ii. Kuanzisha mashamba darasa ya wafugaji nyuki (manzuki);<br>iii. Kufanya mikutano ya wadau, kuwaunganisha wazalishaji wa mazao ya nyuki na masoko; na<br>iv. Kununua gari 1 na pikipiki 5 kwa maafisa wa mradi wa wilaya za Pemba. |
| Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi umetengewa kiasi cha TZS milioni 514.000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo – Umoja wa Ulaya. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa**<br>i. Kutoa mafunzo kwa wafugaji nyuki;<br>ii. Uanzishwaji na uendelezaji wa mashamba darasa ya wafugaji nyuki (manzuki), na<br>iii. Kuwaunganisha wazalishaji wa mazao ya nyuki na masoko. |

**Kiambatanisho Nam. 8H: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo**

| |
|---|
| Kwa mwaka 2023/2024 Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS Bilioni 2.000 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - SMZ |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kujenga chinjio na karantini, kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen kwa ajili ya kuhifadhia mbegu za madume wa ng'ombe. |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi**<br>1. Kuimarisha miundo mbinu ya mifugo kwa kutoa huduma bora kwa jamii. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Serikali**<br>i. Kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen; na<br>ii. Kukarabati na kujenga miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba.<br>iii. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti Kizimbani – maabara, mabanda ya mbuzi na ofisi. |

**Kiambatanisho Nam. 9: Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Programu kwa Mwaka 2023/2024**

